Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili. Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

# Kubainisha Kanuni na Sheria Zinazotawala Muundo wa Maneno katika Sentensi Sahili ya Ekegusii.

**Wilfrida Kemuma.**
**Mount Kenya University, Kenya.**
**Email: winniekemuma@gmail.com**

## IKISIRI

Utafiti huu unalenga kubainisha kanuni na sheria zinazotawala muundo wa maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii. Utafiti huu ulihasisiwa na nadharia ya Sintaksia Finyizi. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani, vitabu teule vya Ekegusii kwa kutumia kifaa cha kudondoa data ulitumika katika kusanya data. Mbinu ya usampulishaji kwa lengo maalum ilitumika kwa lengo la kupata sentensi ambazo hudhihirisha mageuzi. Data iliwasilishwa kwa njia za maelezo. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa muundo wa sentensi unahusu mpangilio wa viambajengo katika sentensi. Muundo wa virai ya sentensi sahili ya Ekegusii unategemea majopo ya maneno kisarufi. Majopo ya maneno yaliyotumika katika utafiti huu yanaweza kuainishwa katika makundi wawili: Jopo la leksia na jopo amilifu. Kuna categoria tano za maneno zilizoainishwa katika jopo leksia nazo ni nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kihusishi. Jopo amilifu hutawaliwa na virai vibainishi, virai vipatanishi na virai shamirisho. Utafiti huu unapendekeza kuwa tafiti zaidi zinaweza kufanywa kuhusu sentensi ambatano au changamano. Isitoshe, utafiti wa mageuzi unaweza kufanywa kwa lugha nyingine ili kueleza iwapo kuna matokeo tofauti.

**Maneno muhimu:** Sentensi sahili, muundo wa maneno.

---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------
**How to cite this article in APA.**
Kemuma, W. (2022). Kubainisha Kanuni na Sheria Zinazotawala Muundo wa Maneno katika Sentensi Sahili ya Ekegusii. *Editon Cons. J. Kiswahili, 4*(1), 374-398. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
---------------------------------------------------------------------***---------------------------------------------------------------------



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## UTANGULIZI

Thiong'o (1986) anaelezea kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya lugha na maendeleo ya wanajamii watumizi lugha. Maendeleo haya hutokana na maelewano katika mawasiliano. Kuelewa maumbo ya maneno katika lugha na misingi ya maumbo hayo kutachangia zaidi kuelewa lugha hiyo na kufanikisha mawasiliano na maelewano haya miongoni mwa wazungumzaji wa lugha husika. Kwa mfano, uhamishaji wa maumbo katika sentensi husababisha athari katika sentensi hiyo. Lugha za kienyeji husheheni tamaduni na amali za jamii hiyo. Mtu ni utamaduni wake na lugha kulingana na Ngugi ni mtu. Ili kumwelewa mtu barabara inabidi basi kuifahamu sintaksia ya lugha yake. Waafrika wataeleweka zaidi wanapozitumia lugha zao za kienyeji. Lugha ya Ekegusii ni lugha ya kienyeji ambayo hubeba utamaduni wa Omogusii.Wazo hili lilimpa mtafiti msingi wa kuifanyia utafiti sentensi sahili ya lugha hii ili kuelewa zaidi miundo yake. Mawazo haya ya Thiong'o yalimsaidia mtafiti kufafanua umuhimu wa kuzingatia lugha ya Ekegusii kama sehemu muhimu ya kufafanua sarufi yake, hasa ikizingatiwa kuwa madhumuni makuu ya lugha yoyote ile ni mawasiliano.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1992), kila lugha ina upekee wa muundo na mpangilio wa maneno katika sentensi zake. Kazi za Guthrie (1947-67, 1970/1971) na Nurse (1985) zinaonyesha kwamba barani Afrika mna makundi manne ya lugha nayo ni: *Niger Kordofanian, Nile Saharan, Afro-Asiatic* na *Khoisan*. Lugha za Kibantu ni miongoni mwa lugha katika kundi la *Niger-Kordofanian.* Lugha za Ekegusii na Kiswahili miongoni mwa zingine ziliainishwa kama lugha za nasaba moja. Muundo wa sentensi wa lugha za nasaba moja kama zilivyo Kiswahili na Ekegusii huonekana kufanana. Sifa moja kuu inayoitambulisha lugha za kibantu ni kwamba nomino zake hupangwa kwenye makundi yanayoitwa ngeli na ambayo katika sentensi huonyesha upatanifu wa kisarufi. Kulingana na misingi anuwai iliyowekwa na wataalam kuhusu sarufi, kila lugha ina vikwazo na kanuni zinazofuatwa katika matumizi yake. Baadhi ya kanuni hizi zimeelezwa kuwa bia na husababisha kuwepo kwa miundo mbalimbali ya sentensi katika lugha mbalimbali. Suala la ugeuzaji wa maumbo ya maneno ni msingi mojawapo ambao huathiri miundo ya sentensi. Kwa misingi ya tafiti za awali katika lugha nyinginezo, utafiti huu unajaza pengo la kubainisha kanuni na sheria zinazotawala muundo wa maneno katika sentensi sahili ya lugha ya Ekegusii.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne 21 Lorghorn (2011) sintaksia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchanganuzi, mpangilio na uhusiano wa vipashio katika sentensi. Kwa mujibu wa Kapinga (1983) sintaksia ni ngazi mojawapo ya ngazi za isimu iliyo kati ya mofolojia na semantiki na huchunguza muundo wa sentensi ya lugha na viambajengo vyake kama vile mofu, maneno, virai na vishazi. Vipashio hivi vina uhusiano mkubwa na huungana katika kuunda kipashio kinachoitwa sentensi. Taaluma hii inahakiki namna maneno yanavyopangwa ili kuunda tungo na sentensi zenye maana katika lugha. Hivi ni kumaanisha kwamba sentensi si kitu kilichopangwa kiholela bali ni mpangilio wa kidaraja unaofuata utaratibu maalum. Utafiti huu kwa hivyo ulinuia kubainisha hizo kanuni na sheria zinazotawala muundo wa maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii ili kubainisha wazi utaratibu huo.

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) kitengo cha sintaksia kina vijitengo viwili. Kwanza kuna kijitengo msingi na pili kuna kijitengo geuzi. Fasiri hizi zilimpa mtafiti mwongozo wa kiwango cha isimu ambacho kilishughulikiwa mbali na kumpa msingi bora wa kufanyia utafiti. Pili ni kuwa fasiri hizi ziliainisha mwongozo wa mpangilio wa maneno katika sentensi ya Ekegusii na kuchunguza ikiwa mpangilio huu ungeafikiana na ile mipangilio ya Kiingereza iliyozungumziwa na hawa waandishi. Kwa mujibu wa waandishi hawa sentensi sahili ni sentensi ambayo ina kitenzi kikuu kimoja na kishazi kimoja na huwakilisha wazo moja tu.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Kijitengo msingi ndicho chenye sheria cha miundo virai. Hiki huonyesha jinsi sentensi zinavyoundwa katika lugha. Kulingana na Bornstein (1978) sheria za miundo virai ni sheria zinazoonyesha kuandikwa tena kwa viambajengo. Hizi sheria ambazo zinaweza kuzalisha sentensi katika lugha huitwa sheria miundo virai. Viambajengo hivi huunganishwa kwa kufuata kanuni fulani. Taaluma ya sintaksia huchunguza kategoria mbalimbali za maneno kulingana na utendakazi wake katika sentensi. Kategoria hizi ni nomino, viwakilishi, vitenzi, vihusishi, vielezi, viunganishi, vivumishi na vihisishi; Hizi ndizo kategoria ambazo hutumiwa katika sentensi. Kategoria hizi ndizo hutumika katika uundaji wa maneno. Kunazo sheria ambazo hufuatwa katika uundaji wa sentensi, kwa mfano, sentensi ya Kiswahili hufuata muundo wa NVTE (Nomino + kivumishi + kitenzi + kielezi).

Kuna waandishi wengi ambao wameyashughulikia masuala ya sintaksia kwa njia mbalimbali. Miongoni mwao ni Chomsky (1986), Napoli (1993), Radford (1997), Culicover (1967) na Poole (2002). Maandishi haya yoye yalisaidia katika kutekeleza malengo ya utafiti huu huku yakitumika kama marejeleo. Kwa mujibu wa Chomsky (1986), kwa mfano, nadharia geuzi ina vitengo vitatu: Fonolojia, sintaksia na semantiki. Kitengo cha sintaksia hushughulikia uundaji wa sentensi. Kitengo hiki ni muhimu katika kazi yetu kwani ndicho kinachoshirikisha sauti za lugha na maana kupitia miundo mbalimbali ya kisintaksia. Aidha, kijitengo geuzi ndicho kinachogeuza sentensi kutoka muundo wa ndani hadi wa nje. Utafiti huu ulinufaika pakubwa na mchango wa wanaisimu hawa. Kijitengo geuzi huhusisha kauli mbili kwa mujibu wa utafiti huu: Kauli tenda na kauli tendwa.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999), lugha za kibantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Aidha, wanaongezea kuwa lugha hizo huwa na mfuatano wa viambishi na mizizi. Viambishi katika lugha hizi huweza kutokea mwanzoni au baada ya mizizi. Baadhi ya sentensi za lugha ya Ekegusii zina sifa mahususi kwa maana kwamba miundo ya sentensi hizo inatofautiana sana na miundo ya lugha za Kinailoti kwa mfano, ambao wamepakana nao, au zile za Ulaya ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zimetumiwa kubuni kanuni za sasa za uchanganuzi wa sentensi.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Muundo wa Sentensi Sahili ya Ekegusii

Sehemu hii ilishughulikia madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ya kubainisha kanuni na sheria zinazotawala muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii. Kwa mujibu wa Radford, (1997) sentensi ni muungano wa virai unaozingatia vigezo vya kisarufi. Muundo huu wa virai hutegemea majopo ya maneno. Kwa mujibu wa Katamba (1993), neno laweza kuwa kiwakilishi cha leksimu kinachohusishwa na sifa za kimofo sintaksia kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, njeo, jinsia na idadi. Neno katika muktadha huu hurejelewa kuwa neno la kimsingi.

Sintaksia Finyizi inaelekeza kuwa maneno yote ya lugha yaainishwe katika kategoria chache cha kisarufi. Dhana ya kategoria za maneno ni istilahiinayotumika katika Sintaksia Finyizi (SF) kurejelea aina mahsusi za maneno yanayoshiriki katika sifa sawa za kisarufi zinazotambulishwa kwa kuzingatia vigezo vya mofolojia , sintaksia na semantiki. Kigezo cha mofolojia, hujihusisha na unyambulishaji wa maneno. Kigezo cha pili cha sintaksia kimejikita katika mpangilio wa maneno katika kishazi au sifa za maneno kuungana katika kishazi husika. Kwa mujibu wa kigezo cha mofolojia na kile cha sintaksia, maneno yanaainishwa katika kategoria nane nazo ni nomino (N), kitenzi (T), kivumishi (V),kielezi (E),kihusishi (H), kibainishi (B) na kishamarishi (SH) (Radford 2009).

Majopo ya maneno ni kategoria za maneno ambazo zina sifa za kisarufi zinazofanana. Upatanisho na unyambuaji wa mofolojia ya maneno ni dhihirisho ya kuwepo sababu ya kutenga majopo ya maneno. Kisarufi majopo ya maneno huweza kuainishwa katika makundi mawili makuu.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

i. Jopo la kileksia
ii. Jopo la kiuamilifu

**Majopo ya kileksia**

Kwa mujibu wa Chomsky (1993) dhana ya jopo leksia hutumika kurejelea jumla ya leksimu zinazopatikana katika lugha fulani. Leksimu ni kipashio kidogo kabisa cha msamiati ambacho kina uwezo wa kubeba maana bila kutegemea kipashio kingine. Jopo la leksia kwa hivyo hujumuisha aina zote za maneno yenye maana leksia. Kuna kategoria tano za maneno zinazoainishwa katika jopo leksia nazo ni: nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kihusishi (Radford, 1997).

**Kategoria ya Nomino**

Kategoria ya nomino hurejelea neno ambalo hutumika kutaja watu, vitu, tabia, hali, matukio, michakato, dhana au mahali. Kategoria finyu za nomino huainishwa kwa kuzingatia ngeli za nomino. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) uainishaji wa ngeli za nomino unafanywa kwa kuzingatia vigezo vitatu ambavyo ni mofolojia, sintaksia na semantiki. Uainishaji wa kisintaksia wa ngeli za nomino ndio unaofaa zaidi katika utafiti huu. Utafiti huu unadhihirisha jinsi nomino inavyohusiana na kitenzi katika sentensi sahili ya Ekegusii. Lugha ya Ekegusii kama lugha zingine za kibantu ina ngeli kumi na tano za nomino. Kwa kuzingatia kigezo cha sintaksia baadhi ya ngeli za nomino za Ekegusii zinaainishwa ifuatavyo (Mbaabu, 1988).

**Jedwali 1: Jedwali la Ngeli za Nomino**

| NGELI | MIFANO YA JINA | MAANA |
|---|---|---|
| O – A | Omonto<br>Abanto<br>Omwana<br>Abana | Mtu<br>Watu<br>Mtoto<br>Watoto |
| E-CHI | Enyomba<br>Chinyomba<br>Echiro<br>Chichiro<br>Enchera<br>Chinchera | Nyumba<br>Nyumba<br>Soko<br>Soko<br>Njia<br>Njia |
| Ri-Ama | Rinyabwari<br>Amanyabwari<br>Rituko<br>Amatuko<br>Richiko<br>Amachiko | Kiazi<br>Viazi<br>Siku<br>Siku<br>Sheria<br>Sheria |
| E – E | Egekoroto<br>Ebikoroto<br>Egetuma<br>Ebituma<br>Egekombe<br>Ebikombe | Kiatu<br>Viatu<br>Hindi<br>Mahindi<br>Kikombe<br>Vikombe |



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
ISSN: 2663-9289
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili*. *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

| | | |
|---|---|---|
| O-AMA | Okogoro<br>Amagoro<br>Okoboko<br>Amaboko | Mguu<br>Miguu<br>Mkono<br>Mokino |
| O-O | Omorembe<br>Omorembe<br>Obwanchani<br>Obwanchani | Amani<br>Amani<br>Upendo<br>Upendo |

**Asili: Kazi ya Mwanafunzi**

Kwa kuzingatia uainishaji wa kisemantiki, kuna aina tano za nomino.

**Jedwali 2: Jedwali la Aina za Nomino**

| NOMINO | KIGEZO | JINA | MAANA |
|---|---|---|---|
| Nomino za pekee | Majina maalum ya watu, mahali au hadhi | Mungu<br>Winnie<br>Kisumu<br>Asiko | |
| Nomino za dhahania | Hizi hutaja vitu visivyoshikika, vitu vya kufikirika tu. | Amasikani<br>Omogoko<br>Obokendu | Heshima<br>Furaha<br>Baridi |
| Nomino za wingi | Hutaja vitu visivyohesabika | Amariga<br>Amate<br>Amache | Machozi<br>Mate<br>Maji |
| Nomino za jamii | Hutumika kutaja vitu vilivyo katika makundi | Egeikaranso kia abagaka | Kikao cha wazee |
| Nomino za kitenzi-jina | Hizi hutokana na vitenzi | Gotara<br>Koragera<br>Gochiesa | Kutembea<br>Kula<br>Kucheza |

**Asili: Kazi ya Mwanafunzi**

Kwa msingi wa kisintaksia, nomino huainishwa kulingana na namna inavyooana na vitenzi katika sentensi kwa umoja na wingi. Hii huitwa upatanisho wa kisarufi.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

**Jedwali 3: Jedwali la Upatanishi wa Kisarufi**

| NGELI | MIFANO YA UPATANISHO | MAANA |
|---|---|---|
| O – BA | *Omonto **o**chire*<br>*Abanto **ba**chire* | Mtu amekuja<br>Watu wamekuja |
| Yo – chi | *Ebando **yo**omire*<br>*Chibando **chi**oomire* | Hindi limekauka<br>Mahindi yamekauka |
| Ki – bi | *Ekerogo **kia**bunekire*<br>*Ebirogo **bia**bunekire* | Kiti kimevunjika<br>Viti vimevunjika |
| Ri - a | *Riuga **ria**mire*<br>*Amauga **a**amire* | Ua limekua<br>Maua yamekua |

**Asili: Kazi ya Mwanafunzi**

Kutokana na jedwali hili ni dhahiri kuwa aina ya nomino ndiyo hutawala muundo wa sentensi katika upatanisho wa kisarufi.

**Kategoria ya Vitenzi**

Kategoria hii inarejelea neno ambalo huashiria vitendo. Kitenzi kinaweza kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kielezi, kihusishi au nomino. Kitenzi huweza kukubali viambishi vya mnyambuliko, nafsi, ngeli, kauli, idadi na njeo (Mbaabu, 1992).Vitenzi huwa ni vya aina mbalimbali kwa mfano vitenzi vikuu ambavyo hubeba maana kuu ya vitendo na havina viambishi kwa mfano;

(1) (a) *Rara* – lala
(b) *Boka* – amka
(c) *Charoka* – ruka

Kuna pia vitenzi visaidizi ambavyo hutumiwa pamoja na vitenzi vikuu ili kuleta maana iliyokusudiwa katika sentensi. Kwa mfano,

(2) *Are* – kuwa

Vipatanisho hivyo aghalabu hupachikwa kwenye vivumishi na viwakilishi. Kadhalika vitenzi huweza kukaa pekee kama sentensi bila kusaidiwa na maneno mengine. Vilevile kutokana na utafiti huu tumebaini kuwa vitenzi huweza kuambishwa viambishi kadha mathalan vya nafsi na wakati.

*Ogato are gochiesa.*
Ogato alikuwa anacheza

Aina ya tatu ya vitenzi ni vitenzi halisi ambavyo huwa na viambishi awali vya nafsi na njeo.
Kwa mfano;

(3) (a) *Orarire* – amelala
(b) *Agacha* – alikuja

Aina zingine za vitenzi ni vitenzi vishirikishi vipungufu, vitenzi sambamba na vitenzi vishirikishi vikamilifu. Vitenzi vinatekeleza majukumu mengi katika sarufi kwa mfano, vitenzi hubeba viambishi vipatanishi vinavyoashiria hali ya upatanisho. Mbali na hayo vitenzi vya Ekegusii hufungiliwa viambishi mbalimbali. Haya ni kwa mujibu wa kanuni ya utegemezi katika nadharia ya Sintaksia Finyizi. Uchunguzi wa vitenzi katika kazi hii ni muhimu kwa kuwa swala la upatanisho wa kisarufi hudhihirika katika lugha ya Ekegusii. Isitoshe, utafiti huu ulibaini kuwa vitenzi huathiriwa na vipengee vingi vya sentensi kwa mfano, nomino huamua kipatanisho kinachostahili kutumiwa katika sentensi.

**Kategoria ya Vielezi**

Kategoria hii inarejelea kipashio katika sentensi ambacho hutumika kuelezea wakati au mahali ambapo kitendo kinafanyika. Kielezi pia hutoa maelezo jinsi kitendo



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili*. *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

kinavyofanyika au sababu ya kutendeka kwake. Katika sentensi ya Ekegusii kuna aina nne za vielezi; vya mahali, vya wakati, vya namna na vile vya viwango.

**Jedwali 4: Jedwali la Aina za Vielezi**

| Aina za vielezi | Sifa bainishi | Mifano | Maana |
|---|---|---|---|
| vielezi vya mahali | [+mahali] | Ime, echiro, isiko | Ndani, sokoni, nje |
| Vielezi vya wakati | [+wakati ] | Igoro, mambia, kare | Jana, kesho, zamani |
| Vielezi vya namna | [+jinsi] | Buya, bwango | Vizuri, haraka |
| Vielezi vya kiwango | [+idadi] | Mono, ikomi, ake | Sana, kumi, kidogo |

**Asili: Kazi ya Mwanafunzi**

Jedwali la kategoria ya kielezi linabainisha kuwa uanishaji wa kielezi hufanywa kwa kuzingatia uamilifu wake katika sentensi. Uamilifu unabainisha uhusiano uliopo baina ya kitenzi na kielezi katika sentensi kwa kuwa kielezi hutoa ufafanuzi kuhusu kitenzi. Kwa mfano kielezi cha mahali huelezea kunakotendeka kitendo, kile cha wakati hubainisha ni lini kitendo kilitendeka au kitatendeka. Kielezi cha namna hufafanua jinsi kitendo kilitendeka huku vile vya viwango hufafanua ni mara ngapi kitendo kilifanyika. Mbali na kutoa ufafanuzi kuhusu vitenzi, vielezi pia huweza kutoa ufafanuzi kuhusu kivumishi (Mbaabu, 1992).

**Kategoria ya Vivumishi**

Kategoria ya vivumishi inarejelea neno ambalo hudhihirisha sifa za nomino. Kwa hivyo vivumishi huwa na uhusiano wa moja kwa moja na nomino. Sifa ya nomino inayodhihirishwa haina budi kufungamanishwa na nomino husika.

Vivumishi huwa ni vya aina mbalimbali kwa mfano vivumishi vya sifa ambavyo huelezea sifa za nomino.
Kwa mfano:

(4) (a)*Egeticha ekiya* –Shamba nzuri
(b)*Orosana oronene*-Msitu mkumbwa
(c) *Eyanga enyia-* Nguo mpya

Vivumishi vya idadi huelezea idadi ya nomino.
Kwa mfano:

(5) (a) *Rituko erimo* – siku moja
(b) *Abanto abange* – watu wengi
(c) *Abana bonsi-* Watoto wote

Vivumishi viashiria huonyesha mahali ambapo nomino ipo, inaweza kuwa mahali karibu, mbali kidogo au mbali zaidi kwa mfano;

(6) (a) *Embori eye* – mbuzi huyu
(b) *Embori eyio* – mbuzi huyo
(c) *Embori eria* – mbuzi yule

**Kategoria ya Kihusishi**

Kihusishi hurejelea neno lenye uhusiano wa moja kwa moja na kitenzi au nomino. Hii inamaanisha kuwa kihusishi hutumika kukita uhusiano baina ya kitenzi au nomino na vijenzi vingine vya sentensi. Kategoria ya kihusishi inaainishwa katika kategoria finyu mbili ambazo ni kihusishi sahili na kihusishi elezi.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

**Jedwali 5: Jedwali la Kategoria Finyu za Kihusishi**

| Kategoria finyu | Sifa bainishi | Mfano | Maana |
|---|---|---|---|
| Vihusihi sahili | [A +-unganifu] | *O, chia, ria* | Wa, cha, la |
| Vihusishi elezi | [+ elezi] | *Rocheime,ekabatiime*<br>Ang'e na<br>*Are na* | Mtoni, kabatini<br>Karibu na<br>Mbali na |

**Asili: Kazi ya Mwanafunzi**

Kategoria zilizojadiliwa katika sehemu hii zinashiriki sifa moja ya kimsingi; kuwa kategoria husika huwa na maana ya kileksia inayowezesha maneno husika kuingizwa katika kamusi kama vidahizo.

Aina mbalimbali za majopo ya maneno huweza kutumiwa pahala fulani maalum katika virai au sentensi. Maneno mbalimbali katika jopo la majina yanaweza kutumiwa katika sehemu moja kwa mfano;

(7) *Ragira ochire echiro (roche, mogondo)*
*Ragira ameenda sokoni (mtoni, shambani)*

Neno *echiro* 'sokoni' linaweza kubadilishana pahala na maneno mengine katika jopo hili kama vile *roche* mtoni, *mogondo* shambani

Kitenzi pia kinaweza kubadilishana pahala na vitenzi vingine katika kirai au sentensi.

Mfano katika sentensi:

(8) *Nyakundi okumirie (orosire, bwebisire)*
Nyakundi ameshangaa (amechoka, amejificha)

Maneno ya kileksia ambayo yanaweza kuainishwa kama vivumishi pia hubadilishana mahala.

Mfano katika sentensi:

(9) *Amatoke amabese (amaya, amabe)*
Ndizi mbichi (mzuri, mbaya)

Kutokana na mifano iliyojadiliwa tunaona kuwa mbali na vipengele vya kimofolojia vile vya kisintaksia pia vinaweza kudhihirisha aina ya maneno kileksia. Neno likitumiwa kubadilishana pahala na neno kutoka jopo lingine kileksia sentensi itakayoundwa haitakuwa sanifu. Mfano katika sentensi;

(10) a) *Bwari ochire (T)*
Bwari amekuja
b) *Bwari roche (H)*
Bwari mtoni
c) *Bwari omopira (N)*
Bwari mpira

Sentensi za (b) na (c) si sahihi kisarufi.

Sarufi ya Ekegusii lazima izingatie matumizi ya maneno kileksia kwani hii ni hatua moja muhimu katika uundaji wa sentensi. Dhana hii ya mofosintaksia ya kutazama maneno kileksia ni muhimu kwa sababu hutuwezesha kutambua jinsi ambavyo maneno haya huungana ili kuunda sentensi sahihi kisarufi.

**Majopo Amilifu**

Kwa mujibu wa Ashton (1944), jopo hili linajumuisha aina zote za maneno ambayo hayana maana leksia. Hii ina maana kuwa jopo hili hujumuisha maneno ambayo hayana maana inayobainika kwa kiwango cha kuorodheshwa kama leksimu katika kamusi na kutolewa maana. Kimsingi majopo haya hubeba taarifa inayodhihirisha uamilifu wa kisarufi wa aina fulani wa vijenzi vya sentensi. Majopo amilifu hujumuisha kibainishi, kipatanishi na kishamirisho. Vibainishi hurejelea neno linalohusiana na nomino kwa kuashiria sifa ambazo hazijafungamana na nomino ingawa huhusiana na nomino husika kwa namna fulani. Sifa zenyewe zinaweza kuwa idadi ya kitajwa, urejeleshi wa kitajwa, uwakilishi wa kitajwa kwa namna ya kipronomino, umilikishi wa kitajwa au uashiriaji wa kitajwa. Kuna aina sita za vibainishi kama zilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**Jedwali 6: Jedwali la Kategoria za Vibainishi.**

| **Aina ya viambishi** | **Sifa bainishi** | **Mifano** | **maana** |
|---|---|---|---|
| Vibainishi vya pronomino/viwakilishi | Hutumiwa badala ya nomino Viwakilishi nafsi | *Inche,aye ,ere* | Mimi,wewe, yeye |
| Vibainishi vimilikishi | Hubainisha umilikaji wa nomino | *Yaye, yane, riaino* | Chake, yangu, lenu |
| Vibainishi idadishi | Hubainisha idadi ya nomino | *Ebinge,oyomo, bita-no* | Tele,mmoja, tano |
| Vibainishi viashiria | Hubainisha nomino kwa kuashiria | *Eye,eyio,eria* | Hii,hiyo,ile |
| Vibainishi rejeleshi | Hubainisha nomino kwa kuirejelea | *Omonyene Ekenyene* | Mwenyewe Chenyewe |
| Vibainishi Jumlishi | Hubainisha nomino kwa kijumla | *Ondebwensi Kendegionsi* | Yeyote Chochote |

**Asili: Kazi ya mwanafunzi**

Kategoria ya upatanishi hurejelea kiungo katika umbo la kitenzi ambacho hubainisha sifa kama cheo, hali, azma, pamoja na upatanisho wa kisarufi. Vipatanisho ambavyo huwakilisha sifa husika mara nyingi hudhihirika kama viambishi katika umbo la kitenzi. Kategoria ya kipatanishi hudhihirisha kategoria mbili: kipatanishi funge na kipatanishi huru.

**Jedwali 7: Jedwali la Kategoria Finyu ya Kipatanishi**

| Kategoria finyu | Mfano | maana |
|---|---|---|
| Kipatanishi funge | *O**ke**imokirie* <br> *Ba**chi**rorire* | Ame**ki**okota <br> Wame**zi**ona |
| Kipatanishi huru | *Arenge* <br> *Chiarenge* | Alikuwa <br> Zilikuwa |

**Asili: Kazi ya mwanafunzi**

Kulingana na jedwali hili kipatanishi funge hudhihirika kupitia kwa viambishi awali ambavyo hutekeleza dhima ya kipatanisho katika umbo la kitenzi. Upatanisho wa aina hii hudhihirika katika lugha ambishi-bainishi kwa mujibu wa Radford (1997). Nacho kipatanishi huru hudhihirika kupitia kwa kitenzi kisaidizi kwa sababu ndicho hutekeleza dhima ya upatanisho wa kisarufi katika muundo wa kishazi. Mbali na dhima ya upatanisho wa kisarufi, kishazi pia hudhihirisha dhima ya uunganisho ambayo hutekelezwa na kategoria ya shamirisho. Shamirisho huhusisha maneno yanayotumika kutanguliza kishazi kitegemezi au kishazi ambatani katika sentensi. Huwa na kategoria finyu mbili: kishamirishi rejeshi na kishamirishi unganifu.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

**Jedwali 8: Jedwali la Kategoria Finyu za Kishamirisho**

| **Kategoria finyu** | **Mifano** | **Maana** |
|---|---|---|
| Kishamirisho rejeshi<br>Kishamirisha unganifu | *Buna*<br>*Korende, gose, nonya* | Kuwa<br>Lakini, au, ingawa |

**Asili: Kazi ya mwanafunzi**

Kishamirisho rejeshi hutanguliza kishazi tegemezi ilhali kishamirisho unganifu hutanguliza kishazi ambatani. Sehemu hii imewasilisha uchanganuzi wa kategoria za maneno ya Ekegusii. Kategoria tatu zimeainishwa: Kipatanishi, kibainishi na kishamirisho. Kwa jumla imebainika kuwa kategoria za maneno ya Ekegusii zinagawika katika majopo mawili: jopo la leksia na jopo la uamilifu. Majopo haya mawili ni muhimu katika sintaksia kwa mujibu wa kanuni tegemezi muundo inayodai kuwa muundo wa kirai au kishazi hautegemei maneno yenyewe bali kategoria za maneno husika. Sehemu inayofuata inadhihirisha nafasi ya kategoria za maneno katika uundaji wa virai ambavyo ndivyo msingi wa uundaji wa sentensi.

**Miundo ya Virai**

Kirai ni fungu la maneno yanayoungana katika sentensi. Huwa ni sehemu ya maneno ambayo ni sehemu ya sentensi. Huweza pia kufafanuliwa kama vipashio vya kimuundo vyenye zaidi ya neno moja. Neno kuu katika kirai hujulikana kama kichwa cha kirai huku maneno mengine yakitambuliwa kama uchomozi wa kichwa cha kirai husika. Kwa mujibu ya kamusi ya Longhorn (2011) Kirai ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima-kiarifu. Massamba (2004) anadai kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima-kiarifu. Culicover (1976) anadai kuwa kirai ni mfuatano wowote wa maneno katika lugha yoyote na maneno yenyewe ni ya kategoria fulani. Naye Radford (2004) anadai kuwa kila kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai chote. Kirai huainishwa kimuundo kulingana na kichwa cha kirai husika, kwa mfano kirai ambacho neno lake kuu ni nomino huitwa kirai nomino. Kwa kawaida kirai nomino hakihusishi mtenda na kitendo kinachotekelezwa kulingana na mkabala huu tuna aina zifuatazo za virai: virai nomino, virai vivumishi/virai vumishi, virai vielezi/virai elezi, virai vitenzi/virai tenzi na virai vivihusishi/virai husishi

Massamba na wenzake (1999) wameelezea kirai kuwa ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima kiarifu. Muundo wa kiima karifu ni ule ambao unahusisha mtendaji wa tendo na tendo linalotendwa na ambao ndio muundo wa msingi wa sentensi katika lugha yoyote ile. Kirai huundwa na mahusiano maalumu baina ya maneno. Mahusiano hayo huwa ni ya asili katika lugha. Uundaji wa virai umekitwa katika aina za maneno. Kwa hivyo, aina hizo za maneno ndizo hutumika kama msingi wa kuainisha virai. Virai mbalimbali huunda sentensi vinapounganishwa. Uchanganuzi wa sentensi, kwa hivyo, huwa ni uchanganuzi wa mahusiano baina ya vilivyomo ndani yake. Maalumu ndani ya vipashio hivyo. Kwa hivyo virai vinaweza kuianishwa kutegemea aina hizo za maneno. Katika lugha ya Ekegusii tulipata aina kadhaa za virai nazo ni: virai nomino, virai vitenzi,virai vivumishi, virai vielezi na virai viunganishi.

Radford (2009) amesema kuwa kuna viwango vitatu vya kuchanganua virai.

i) Kategoria ya kiwango cha neno,
ii) Kategoria ya kiwango cha kati,
iii) Kategoria ya kiwango cha kirai



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

Kwa mujibu wa Radford (2009), kategoria za kati huwa kubwa kuliko kategoria leksia lakini ndogo kuliko kirai kikuu. Kuna viambajengo vilivyo vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko kirai nomino na jinsi ambayo kuna virai vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko kirai nomino. Hali kadhalika tuna virai vivumishi vilivyo vikubwa kuliko vivumishi lakini vidogo kuliko virai vivumishi vikuu. Tuna virai vielezi vilivyo vikubwa kuliko vielezi lakini vidogo kuliko virai vielezi vikuu. Hali kadhalika tuna virai husishi vilivyo vikubwa kuliko vihusishi lakini vidogo kuliko virai husishi vikuu. Mwisho kuna virai vitenzi vilivyo vikubwa kuliko vitenzi lakini vidogo kuliko virai vitenzi vikuu.

Kila kategori ya kirai ina kategoria leksika. Hii ni sadfa. Kirai nomino ni lazima kiwe na nomino na kitenzi lazima kiwe na kitenzi. Kipashio ambacho ni cha lazima katika kikundi fulani huitwa kichwa cha kategoria. Kuna aina mbili kuu za virai: Kirai leksia na kirai amilifu.

**Kirai Leksia**
Kwa mujibu wa Radford (1997) dhana ya kirai leksia inatumika kurejelea aina zote za virai ambavyo hutokana na kategoria za maneno ambayo kiasilia yana maana ya kileksia. Maneno leksia ndiyo maneno tawala katika kirai hiki. Kuna virai leksia vitano navyo ni: Kirai nomino, Kirai kitenzi, Kirai kivumishi, kirai kielezi na kirai kihusishi.

**Kirai Nomino**
Kirai nomino ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu mengine ya maneno. Muundo wa kirai nomino huwa na kichwa cha nomino kama tawala. Miundo mingine ya kirai nomino ni nomino pamoja na kirai kihusishi. Hali kadhalika, kirai nomino huweza kuwa kiima au yambwa. Kirai nomino huwa na majukumu mbalimbali kisintaksia katika sentensi ya Ekegusii. Kwanza, kirai nomino hutekeleza jukumu la kiima. Kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hutuambia ni nani, kipi, nini kinachozungumziwa katika sentensi. Kirai nomino hutekeleza jukumu la yambwa tendwa. Yambwa tendwa ni nomino ambayo huathiriwa na tendo moja kwa moja.


Katika jukumu la yambwa tendwa, kirai nomino hutaja mtu anayefaidika au kuhasirika na kitenzi.
Tuna miundo mbalimbali ya kirai nomino:

(a)Nomino moja pekee inaweza kuunda kirai.
Mfano katika sentensi:
(11) *Nyakundi bwebisire*
Nyakundi amejificha

(b) *Chinyange chiatwomanire*
Baiskeli zimegongana.

Uwakilishi wa mishale.

KN → N
N → Nyakundi




*Mchoro 1:* Mchoro wa Nomino Moja

(b) Nomino mbili zinaweza kuunda kirai.

Mfano katika sentensi
(12) *Bwari na Ragira bachire.*
Bwari na Ragira wamekuja.

Uwakilishi wa mishale.
S → $N_1$ + U + N2 + T
KN → $N_1$ + U + $N_2$




©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili*. Double –Blind Peer Reviewed Journal

$N_1$ → Bwari
$N_2$ → Ragira





*Mchoro 2:* Mchoro wa Nomino Mbili

(a) Kuna pia muundo wa nomino na kivumishi ili kuunda kirai nomino.

(13) *Omonto oria ogure.*
Mtu yule ameanguka.

Uwakilishi wa mishale

S → KN + KT
KN → N+V
N → Omonto
V → Oria




**Mchoro 3: Mchoro wa Nomino na Kivumishi**

Aina mbalimbali za KN zimebainishwa katika sehemu hii. Kutokana na mifano hii inabainika kuwa kirai nomino kinaweza kuwa na neno moja au fungu la maneno mawili. Pia imebainika kuwa KN kinaweza kubeba virai vingine kama kirai kivumishi na kirai kitenzi.

**Kirai Kitenzi**

Kirai tenzi KT ni kirai kilichokitwa katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Neno tawala hapa huwa ni kitenzi. Kuna miundo mbalimbali ya kirai tenzi katika sentensi ya Ekegusii.

a) Kitenzi pekee.
Mfano katika sentensi:

(14) *Twomana.*
Gongana.

Uwakilishi wa mishale

S → KT
KT → *Twomana*

KT

T

*Twomana*

**Mchoro 4: Mchoro wa Kitenzi Pekee**

b) Kitenzi na nomino moja
Umbo la kitenzi na nomino linawakilishwa kwa sheria: KT → T + N

Mfano katika sentensi:

(15) *Obwatire omonwa.*
Ameshika mdomo.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

KT

T N

*Obwatire Omonwa*


**Mchoro 5: Mchoro wa Kitenzi na Nomino**

c) Kirai kitenzi na nomino mbili

(16) *Akaa Regina ebituma.*
Akampa Ragina mahindi.

Uwakilishi wa mishale


| | |
|---|---|
| KT | $T + N_1 + N_2$ |
| T | Akaa |
| $N_1$ | Ragina |
| $N_2$ | ebituma |




**Mchoro 6: Mchoro wa Kitenzi na Nomino Mbili**

d) Kirai kitenzi vile vile huunda kirai kitenzi.


Mfano katika sentensi:
(17) *Ochire Komokonya.*
Amekuja kumsaidia.




**Mchoro 7: Mchoro wa Vitenzi Viwili**

e) Kitenzi na kielezi huunda kirai kitenzi

Mfano katika sentensi:
(18) *Ochire bwango.*
Amekuja haraka.




**Mchoro 8: Mchoro wa Kitenzi na Kielezi**



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org


Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

f) Kitenzi, nomino na kitenzi huunda kirai kitenzi
Mfano katika sentensi:
(19) *Agatebia Bwari aminyoke.*
Alimwambia Bwari akimbie.





**Mchoro 9: Mchoro wa Kitenzi, Nomino na Kitenzi**

**Kirai Kivumishi**

Muundo wa kirai hiki umekitwa katika kivumishi. Kwa hivyo, muundo wa kirai kivumishi una kivumishi kama kichwa chake pamoja na maneno mengine yanayotawaliwa na kivumishi. Kirai kivumishi hufafanua nomino au kiwakilishi chake na kwa hivyo kufanya kazi kama kivumishi kimoja kifanyavyo. Kirai kivumishi hujikita katika kirai nomino ingawa wakati mwingine upatikana pamoja na kirai kitenzi kishirikishi. Hata hivyo ni muhimu kusisitiza kuwa kirai kivumishi huwa na muundo uliobainika. Tuna aina mbalimbali za kirai kivumishi kwa mfano kivumishi pekee, kivumishi na kivumishi kingine, na kivumishi na nomino. Maumbo yafuatayo yanadhihirika katika sentensi ya Ekegusii.


a) Kivumishi na kielezi
Mfano katika sentensi:
(20) *Emwamu mono.*
Nyeusi kabisa.

Uwakilishi wa mishale.
KV V + E
V *emwamu*
E *mono*
KV




**Mchoro 10: Mchoro wa Kivumishi na Kielezi**

b) Kivumishi na nomino.
Mfano katika sentensi:
(21) *Omonyene enyange.*
Mwenye baisikeli.
Uwakilishi wa mishale.
KV → V + N
V *omonyene*
N → *enyange*




**Mchoro 11: Mchoro wa Kivumishi na Nomino**


Kivumishi na kirai nomino vile vile huunda kirai kivumishi
Mfano katika sentensi:
(22) *Omonyene enyange eyio.*



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org


Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

Mwenye baiskeli hiyo.
Uwakilishi wa mishale.
KV → V + KN
V omonyene
KN → enyange eyio





**Mchoro 12: Mchoro na Kivumishi na Kirai Nomino**

c) Kivumishi na kirai tenzi vile vile huunda kirai kivumishi
Mfano katika sentensi:
(23) Oyo *ominyogete bwango.*
Mwenye kukimbia haraka.
Uwakilishi wa mishale.
KV V + KT
V oyo
KT *ominyogete bwango*




**Mchoro 13: Mchoro wa Kivumishi na Kirai Tenzi**

**Kirai Kielezi**
Kirai kielezi ni kirai chenye muundo wa maneno mawili au zaidi yanayofanya kazi kwa pamoja kama kielezi. Kirai kielezi hubeba habari inayotumika kufafanua kitenzi, kivumishi au hata kielezi kingine. Kirai kielezi hueleza jinsi kitu kilivyofanyika, mahali kilipofanyika au wakati (Habwe na Karanja, 2004). Kirai kielezi huweza kuwa vya mahali, vya namna au hali, vya idadi au kiwango na vya wakati. Aghalabu hushika nafasi baada ya kitenzi katika sentensi.
Mfano katika sentensi:
(24) *Buya mono*
Vizuri sana




**Mchoro 14: Mchoro wa Kirai Kielezi**


Kinyume na aina zingine za virai, muundo wa kirai kielezi hauelekei hukitwa kwenye mahusiano ya lazima baina ya neno kuu (kielezi) na neno au fungu la maneno linaloandamana nalo. Badala yake, kirai kielezi kinaundwa kwa maneno mawili na ambayo yote yanahitajika kuwa kielezi. Kirai kielezi huweza kuundwa kwa kielezi pekee, vielezi zaidi ya kimoja na kielezi na kirai husishi
Mfano katika sentensi:
(25) *Mambia mono.*
Asubuhi sana.
Uwakilishi wa mishale.


©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

KE → $E_1 + E_2$
$E_1$ → mambia
$E_2$ → mono




**Mchoro 15: Mchoro wa Kirai Kielezi**

**Kirai Kihusishi**

Hiki ni kirai ambacho kichwa chake ni kihusishi. Muundo wa kirai kihusishi hukitwa katika mahusiano baina ya kihusishi na fungu la maneno linaloandamana nacho. Maumbo ya kirai kihusishi yanayodhihirika katika Ekegusii ni; kihusishi na nomino, kihusishi na kirai nomino, kihusishi na kira kielezi. Kihusishi huwa na sehemu ya kundi tenzi ambapo hufanya kazi kama kielezi. Ikiwa kirai kihusishi kitajiri kama viambajengo vya kundi nomino basi hutekeleza kazi kama kivumishi. Kirai kihusishi uweza kutokea popote katika sentensi kwa mfano mwanzoni na mwishoni mwa sentensi. Kirai kihusishi hutekeleza majukumu kadha katika sentensi. Kwanza hutumiwa kufafanua nomino (kama kivumishi). Pili kirai kihusishi (KH)

Hutumiwa kufafanua vitenzi (kama kielezi) na mwisho hutumiwa kama kiwakilishi. Kirai kihusishi hujitokeza katika miundo mbalimbali kwa mfano kihusishi na kielezi na kihusishi na nomino katika sentensi sahili.

Kihushisi na nomino

Mfano katika sentensi:


(26) a) *Isiko ye' kanisa*
Nje ya kanisa
b) *Nyaro ye' getanda*
Chini ya kitanda

Aghalabu kirai kihusishi hutangulia nomino;

Uwakilishi wa mishale

KH → H + N
H → isiko ye'
N → kanisa

(34) Uwakilishi wa mchoro matawi




**Mchoro 16: Mchoro wa Kirai Kihusishi**

Sehemu hii imewasilisha miundo mbalimbali ya virai leksia. Virai leksia huangazia maana msingi ya sentensi na ili kuzalisha tungo ndefu, virai leksia hushirikiana na virai amilifu.

**Virai Amilifu**

Dhana ya virai amilifu inatumika kurejelea kundi la virai ambavyo vina muundo uliokitwa katika uhusiano baina ya kategoria amilifu za maneno na maneno mengine. Virai hivi ni vikubwa zaidi ya virai leksia kwa sababu huunganisha neno tawala na virai vingine au majopo mengine ya maneno leksia. Virai hivi hutawaliwa na maneno kutoka



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

kwenye jopo amilifu ambayo ni virai vibainishi, virai vipatanishi na shamirisho.

**Virai Vibainishi**

Dhana ya kirai kibainishi inarejelea kirai chenye kichwa cha kibainishi. Kibainishi huungana na kategoria zingine za maneno na kuzua maumbo mbalimbali ya kirai kibainishi. Katika Ekegusii maumbo yafuatayo ya vibainishi hudhihirika;

a) Umbo la kibainishi pekee

Hili huwakilishwa kwa sheria; KB B.

Hapa umbo la kirai bainishi linajumuisha kibainishi kimoja pekee.

Mfano katika sentensi:


(27) *Barabwo*

Wao

Uwakilishi wa mishale.

KB → B

B → *Barabwo*




**Mchoro 17: Mchoro wa Kirai Kibainishi**

b) Umbo la vibainishi viwili

Mfano katika sentensi:

(28) *Intwe twensi*


Sisi sote

Uwakilishi wa mishale.

KB → B + B

B → *Intwe*

B → *Twensi*




**Mchoro 18: Mchoro wa Vibainishi Viwili**

c) Umbo la kibainishi na nomino

Mfano katika sentensi

(29) *Abwo echiro*


Hapo sokoni

Uwakilishi wa mishale.

KB → B + N

B → *abwo*

N → *echiro*




Mchoro 19: Mchoro wa Kibainishi na Nomino

d) Umbo la kibainishi na kirai nomino.

Mfano katika sentensi:

(30) *Inwe abana abake*

Ninyi watoto wadogo

Uwakilishi wa mishale.

KB → B + KN

B *Inwe*

KN N + V

N *abana*

V *abake*




©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal





**Mchoro 20: Mchoro wa Kibainishi na Kirai Nomino**

e) Umbo la kirai kibainishi na kirai kihusishi

Mfano katika sentensi:
(31) *Ebio bia mogondo.*
Hizo za mashamba.
Uwakilishi wa mishale

KB → B + KH
B *Ebio*
KH → H+N
H → *bia*
N → *mogondo*




**Mchoro 21: Mchoro wa kibainishi na Kirai Kihusishi**

Mifano hii inadhihirisha kwamba kibainishi huweza kuungana na kategoria nyingi za maneno kuunda kirai finyu au panzi zaidi.


**Kirai Patanishi**

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004), dhana ya kirai patanishi inarejelea kirai ambacho kichwa chake ni kipatanishi. Kirai patanishi hukitwa katika mahusiano baina ya kipatanishi na kategoria ya kitenzi katika muundo wa kishazi. Maumbo ya kirai kipatanishi huweza kufanyiwa uchomozi ili kuibua KP panuzi ambacho hubeba virai vingine;

Mfano katika sentensi:

a) Umbo la kirai kipatanishi funge

(32) *Chigatwomana*
Zikagongana
Uwakilishi wa mishale
KP P + T
P *chiga*
T *twomana*




**Mchoro 22: Mchoro wa Kirai Kipatanishi Funge**

b) Umbo la kirai kipatanishi panuzi

Mfano katika sentensi:
(33) *Ekamotwoma omogaka oyio.*
Ikamgonga mzee huyo.

Uwakilishi wa mishale

KP → P+KT+KN
P → *ekamo*
KT → T
T → *twoma*
KN → N+B




©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

N *omogaka*
B *oyio*




**Mchoro 23: Mchoro wa Kirai Kipatanishi Panuzi**

**Kirai Shamirisho**

Dhana kirai shamirisho inarejelea kirai ambacho kichwa chake ni kishamirisho. Kirai shamirisho ni kikubwa kuliko virai vingine. Muundo wa shamirisho hukitwa katika mahusiano ya kishamirisho na maneno mengine katika kishazi. Kirai shamirisho vilele kinarejelea kiungo cha uamilifu wa kisintaksia ambacho huungana na kiarifu ili kuunda kiungo kikubwa zaidi na huja kabla ya kiarifu.

a) Umbo finyu la kirai shamirisho

Umbo husika linawasilishwa kwa sheria.

KSH SH + T

Mfano katika sentensi:

(34) *Na koonia.*


Na kuuza.

Uwakilishi wa mishale.

KSH SH+T

SH → *na*

T → *koonia*




Mchoro 24: Mchoro wa Kirai Shamirisho

b) Umbo panuzi la kirai shamirisho hujumuisha kishamirisho na kirai tenzi :

SH SH+KT


Mfano katika sentensi:

(35) *Na koonia engoko.*

Na kuuza kuku.

Uwakilishi wa mishale

KSH SH+KT
SH na
KT T+N
T *koonia*
N engoko






©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

*Mchoro 25: Mchoro wa Kirai Shamirisho na Kirai Tenzi*

c) Umbo la shamirisho na kirai patanishi


Mfano katika sentensi:

(36) *Onye gakoonia.*

Ikiwa atauza.

Uwakilishi wa mishale

KSH → SH+KP
SH → Onye
KP → P+T
P → gako
T → onia




**Mchoro 26: Mchoro wa Kirai Shamirisho na Kirai Patanisho**

Sehemu hii imeshughulikia namna ambavyo virai mbalimbali huundwa. Muundo wa virai ndiyo msingi wa uundaji muundo wa sentensi zilizo na maana. Utaratibu fulani ni lazima, kwa hivyo, ufuatwe ili kuunda sentensi zilizo na maana.

**Muundo wa sentensi ya Ekegusii**

Sentensi ni neno au fungu la maneno linalotoa habari kamili. Kwa mujibu wa sintaksia virai, maneno ya lugha hujiunga pamoja ili kuunda virai vyenye maana ya kisarufi. Virai hivi navyo hujiunga ili kuunda sentensi. Jinsi ilivyo katika lugha zingine za kibantu, sentensi za Ekegusii huchukua muundo wa KN na KT


Mfano katika sentensi:

(37) *Etigere yasombire ebituma.*

Punda amesomba mahindi.

Uwakilishi wa mishale

S → KN + KT
KN → N
N → *Etigere*
KT → T+N
T → *yasombire*
N *ebituma*




Mchoro 27: Mchoro wa Muundo wa Sentensi ya Ekegusii

(38) Uwakilishi wa mishale

KSH → SH+KP
SH → Onye
KP → P+T
P → gako
T → onia

(38) *Nyakundi bwebisire*

Nyakundi amejificha

Uwakilishi wa mishale.

S → KN + KT
KN N
N Nyakundi
KT T
T bwebisire



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

Uwakilishi wa mchoro matawi

S

KN KT

N T


*Nyakundi bwebisire*

**Mchoro 28: Mchoro wa Muundo wa Nomino na Kitenzi**

(39) *Omonto oria ogure nse*

Mtu yule ameanguka chini

S → KN + KT
KN → N+V
N → *Omonto*
V → *oria*
KT → T+E
T → *ogure*
E → *nse*




*Omonto oria ogure nse*


**Mchoro 29: Mchoro wa kundi nomino na kundi tenzi**

(40) *Bwari na Ragira bagauta omorero*

Bwari na Ragira waliwasha moto

Uwakilishi wa mishale.

S → KN + KT
KN → N +U+N
N → Bwari
U → na
N → *Ragira*
KT → T+N
T → *bagauta*
N → *omorero*




Mchoro 30: Mchoro Kundi Nomino (N1 + U + N) na KT ( T + N2)

Kuna muundo wa sentensi ya neno moja ambalo huwakilisha nafsi, wakati na kitenzi, kwa mfano:

(41) Agakumia → A + ga + kumia →




©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*


Akashangaa A + ka + shangaa




**Mchoro 31: Mchoro wa Muundo wa Sentensi ya Neno Moja**

Leksia na virai amilifu hufungamana ili kuunda kirai kikubwa zaidi yaani sentensi.
Mfano katika sentensi:
(42) *Omwana orarire.*
Mtoto amelala.

Uwakilishi wa mishale
KP → KN + KT
KN → *Omwana*
KT → *Orarire*





*Omwana* *o* *rarire*

**Mchoro 32: Mchoro wa Leksia na Virai Amilifu**
(43) *Origereirie nyuma*
Ameangalia nyuma
Uwakilishi wa mishale

KP KT + E
KT *origereirie*

KE *nyuma*






©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

**Mchoro 33: Mchoro wa Kirai Patanishi**

Vilevile kuna miundo ya sentensi ambayo sehemu ya nomino huamilisha kiima na kirai kitenzi huamilisha kiarifu shamirisho chagizo.

Mfano katika sentensi:

(44) *Bwari agetweka ebituma*

Bwari akajitwika mahindi.

Kiima kiarifu shamirisho

45) *Ragira akabogoria ebituma bionsi*

Ragira akabeba mahindi yote

Kiima kiarifu shamirisho chagizo

**Mchoro 34: Michoro ya Miundo ya Kiima na Shamirisho**

Sentensi za Ekegusii huongozwa na kanuni bia ambazo ni kanuni leksia na utegemezi muundo na kanuni mahsusi ambayo ni upatanishi wa kisarufi. Katika upatanishi wa kisarufi ngeli ya nomino huathiri kiambishi awali cha kitenzi katika sentensi husika. Kwa mujibu wa Cook na Newson (1966) miundo ya sentensi hutegemea aina ya majopo ya maneno yaliyotumiwa na hasa kiima na kiarifu. Jambo hili linadhihirika wazi katika sentensi za Ekegusii.


Mfano katika sentensi:

(46) ***E***twoni ***e***mwamu ***ya***sirire

Jogoo mweusi amepotea

***Chi***twoni ***chi***mwamu ***chi***asirire

Jogoo weusi wamepotea




**Mchoro 35: Michoro ya Miundo ya Kiima na Shamirisho**

Katika mfano huu kiima huathiri kiambishi awali cha kivumishi na kitenzi. Viambishi `e' na `chi' katika mfano huu hudhihirisha ule upatanishi wa kisarufi. Majopo leksia na majopo amilifu hushirikiana ili kuunda sentensi zenye miundo mbalimbali za Ekegusii. Kwa mujibu wa Chomsky (1995) Sintaksia Finyizi inatawaliwa na kanuni au mihimili sita. Mihimili ya nadhalia inayotumika hapa ni ile ya ufasiri kamili ambapo kuna mashiko kuwa kila kijenzi cha kisarufi lazima kifasirike kwa maana bayana ya kileksia na kisarufi.

Uchanganuzi wa sentensi za Ekegusii umedhihirisha kuwa sentensi hizo huundwa kutokana na majopo ya maneno



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kisarufi. Majopo hayo ni leksia na amilifu. Majopo leksia huhusisha maneno kama vile nomino, kivumishi, kitenzi, kielezi, vihusishi pamoja na virai vyao. Nayo majopo amilifu huhusisha vibainishi, viunganishi na shamirisho au yambwa. Muundo wa virai vya Ekegusii vile vile umejadiliwa. Virai vya Ekegusii vimedhihirika kuundwa kutokana na maneno leksia. Katika kuunda kirai, imedhihirika kuwa maneno hayo huungana na lile neno tawala likawa ndilo linaunda kirai husika. Utafiti wetu ulipata virai leksia vitano ambavyo ni: kirai nomino, virai vivumishi, virai vitenzi, virai vihusishi na virai vielezi. Virai amilifu navyo ni vitatu kutokana na matokeo ya utafiti huu: virai viunganishi, virai vibainishi na virai shamirisho. Hizi aina mbili za virai leksia na amilifu huungana ili kuunda virai vikubwa zaidi ambavyo ni sentensi. Majopo ya maneno ni lazima yahusiane vizuri kwa kufuata sheria za uudaji wa sentensi ili kuunda sentensi sahihi. Miundo ya sentensi hutegemea virai vilivyotumiwa katika kuziunda. Sentensi iliyoshughulikiwa katika utafiti huu ni sentensi sahili.

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Mahitimisho:** Muundo wa sentensi unahusu mpangilio wa viambajengo katika sentensi. Muundo wa virai ya sentensi sahili ya Ekegusii unategemea majopo ya maneno kisarufi. Majopo ya maneno yaliyotumika katika utafiti huu yanaweza kuainishwa katika makundi wawili: Jopo la leksia na jopo amilifu. Kuna categoria tano za maneno zilizoainishwa katika jopo leksia nazo ni nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kihusishi. Jopo amilifu hutawaliwa na virai vibainishi, virai vipatanishi na virai shamirisho.

**Mapendekezo:** Kutoka na utafiti huu mtafiti anapendekeza kuwa tafiti zaidi zinaweza kufanywa kuhusu sentensi ambatano au changamano. Isitoshe, utafiti wa mageuzi unaweza kufanywa kwa lugha nyingine ili kueleza iwapo kuna matokeo tofauti.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

**DOI:** https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.357
**Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|**
**Received: 05.04.2022; Accepted 10.04.2022; Published on 20.04. 2022 at www.editoncpublishing.org**
**Kemuma, W., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

**MAREJELEO**

Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar*. Longman Group Limited.
Bornstein, D. (1978). *An Introduction to Transformational Grammar*. Winthrop Publishers.
Chomsky, N. (1986). *Barriers*. M.T.I Press.
Chomsky, N. (1993). *A Minimalist Program for Linguistic Theory* in K. Hale S. J. Keyser (eds). *The View from Building 20 Essays in Linguistics in Honour of Sylvai Brombergers.* M.T. I Press.
Chomsky, N. (1995).*The Minimalist Programme.* M.T. I Press.
Cook, V. J., & Newson. (1996). *Chomsky's Universal Grammar:* (2nd Ed). Basil Blackwell.
Culicover, P.W. (1967). *Syntax*. Academic Press.
Guthrie, M. (1948). *Classification of Bantu Languages*. Oxford University Press.
Guthrie, M. (1971). *Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative Linguistics Pre-History of the Bantu Language* 2. Gregy Press.
Habwe, J. H., & P. Karanja (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Phoenix Publishers.
Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. TUKI.
Katamba, F. (1993). *An Introduction to Phonology*. Longman.
Longhorn (2011). Kamusi ya Karne 21. Longhorn.
Massamba, D. P. B., Kihore Y. M., & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu.* TUKI.
Massamba, D. P. B., Kihore Y. M., & Hokororo, J. I. (2004). Kamusi ya Falsafa na Isimu. TUKI.
Mbaabu, I. (1988).*Kiswahili Lugha ya Taifa*. KLB.
Mbaabu, I. (1992). *Sarufi ya Kiswahili*. Longman Kenya.
Napoli, D.J. (1993). Syntax: Theory and Problems. Oxford University Press.
Nurse, D., & Philipson, G. (1980).*The Bantu Languages*. Routledge
Poole, G. (2002). *Syntatic Theory.* Hampshire, Palgrave.
Radford, A. (1997). *Syntax: A Minimalist Introduction*. M.T.I Press.
Radford, A. (2009).*Transformational Grammar. A First Course*. Cambridge University Press.
Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind*: The Politics of Language in African Literature. J. Currey.



©2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org